



Mark Scheme (Results)

Summer 2025

Pearson Edexcel International GCSE
In Swahili (4SW1) Paper 02
Listening

Edexcel and BTEC Qualifications

Edexcel and BTEC qualifications are awarded by Pearson, the UK's largest awarding body. We provide a wide range of qualifications including academic, vocational, occupational and specific programmes for employers. For further information visit our qualifications websites at www.edexcel.com or www.btec.co.uk. Alternatively, you can get in touch with us using the details on our contact us page at www.edexcel.com/contactus.

Pearson: helping people progress, everywhere

Pearson aspires to be the world's leading learning company. Our aim is to help everyone progress in their lives through education. We believe in every kind of learning, for all kinds of people, wherever they are in the world. We've been involved in education for over 150 years, and by working across 70 countries, in 100 languages, we have built an international reputation for our commitment to high standards and raising achievement through innovation in education. Find out more about how we can help you and your students at: www.pearson.com/uk

Summer 2025

Question Paper Log Number P78565

Publications Code 4SW1_02_2506_MS

All the material in this publication is copyright

© Pearson Education Ltd 2025

General Marking Guidance

- All candidates must receive the same treatment. Examiners must mark the first candidate in exactly the same way as they mark the last.
- Mark schemes should be applied positively. Candidates must be rewarded for what they have shown they can do rather than penalised for omissions.
- Examiners should mark according to the mark scheme not according to their perception of where the grade boundaries may lie.
- There is no ceiling on achievement. All marks on the mark scheme should be used appropriately.
- All the marks on the mark scheme are designed to be awarded. Examiners should always award full marks if deserved, i.e. if the answer matches the mark scheme. Examiners should also be prepared to award zero marks if the candidate's response is not worthy of credit according to the mark scheme.
- Where some judgement is required, mark schemes will provide the principles by which marks will be awarded and exemplification may be limited.
- When examiners are in doubt regarding the application of the mark scheme to a candidate's response, the team leader must be consulted.
- Crossed out work should be marked UNLESS the candidate has replaced it with an alternative response.

Question number	Answer	Mark
1(a)	F	(1)
1(b)	H	(1)
1(c)	C	(1)
1(d)	B	(1)

Question number	Answer	Mark
2	C, F	(2)
	D, A	(2)
	E, G	(2)

Question number	Answer	Mark
3(a)	wachapakazi NA Washindani / kupita mtihani / kupita mtihani	(2)
3 (b)	Kazi za shule / kazi ya ziada	(1)
3(c)	mwalimu	(1)
3(d)	Kaa nyumbani / pumzika NA Tafuta kazi / kupata kazi	(2)

Question number	Answer	Mark
4(a)	Chanya (+) na Hasi (-)	(1)
4(b)	Chanya (+)	(1)
4(c)	Chanya (+)	(1)
4(d)	Hasi (-)	(1)
4(e)	Hasi (-)	(1)
4(f)	Chanya (+) na Hasi (-)	(1)

Question number	Answer	Mark
5(a)	A saa	(1)
5(b)	B ana kwa ana	(1)
5(c)	D mshangao	(1)
5(d)	C maisha yetu	(1)
5(e)	C mwezi	(1)
5(f)	B umejuta ulichosema	(1)

Question number	Answer	Mark
6(a)	B	(1)
6(b)	E	(1)
6(c)	D	(1)
6(d)	F	(1)
6(e)	H	(1)
6(f)	A	(1)

Question number	Answer	Accept	Reject	Mark
7(a/ b)	Any two of: (Huzurura) karibu na mto AND/OR Kuvua dagaa AND/OR Kujuana vizuri		marafiki	(1) (1)
7(c)	Hakuna faragha	Shule za sekondari zipo mbali Watu kujua yote Faraha (spelling)	Furaha/ faraka	(1)
7(d)	kuenda kwenye darasa la muziki			(1)
7(e/f)	Usafiri wa umma (una umati mkubwa) AND/OR Uchafuzi wa hali ya hewa AND/OR Msongamano wa magari		uchafu	(1) (1)



Pearson

Transcript of Listening Test

Summer 2025

Pearson Edexcel International GCSE
in Swahili (4SW1/02)

Paper 2 Listening

Wapi nyumbani?

Question 1

Example

F1 Funguo zipo jikoni.

Question 1 Part (a)

M1 Wageni wameshafika na wamekaribishwa sebuleni kwetu.

Question 1 Part (b)

F2 Mama yangu amenifundisha kutandika kitanda ninapoamka tu.

Question 1 Part (c)

M2 Jua lilipokuwa kali sana, tulikaa nje barazani halafu tukanywa chai.

Question 1 Part (d)

F1 Muhimu kukoga kila asubuhi kwa kutumia maji ya moto au baridi.

Shughuli wakati wa mapumziko

Question 2

Example

M1 Hannah, hivi unapenda kufanya nini wakati wa mapumziko?

F1 Mimi ninapenda kusoma vitabu vya riwaya.

Questions

M1 Na wewe je, Mikaeli?

M2 Mimi sivutiwi kabisa na kuogelea. Ninavutiwa na michezo ambapo ninaweza kukaa kwenye kiti na kutumia akili yangu. Ninapenda bao ingawa wakati wa jioni hucheza karata na familia yangu.

M1 Kumbe! Na wewe je, Aaliyah?

F2 Tangu utotoni, wazazi wangu walikuwa wakinipeleka kucheza mpira wa kikapu. Ninaupenda mchezo huo na pia kwa vile nina miguu mirefu husikia raha kukimbia.

F1 Na wewe, Omari,?

M1 Sipendi michezo inayohitaji kuwa katika timu kwa hivyo mimi huchora picha ninapokuwa nyumbani ingawa ninavutiwa zaidi na kupiga picha za mazingira.

Masomo na Ajira

Question 3

F2

Mimi ni Asha. Rafiki zangu shuleni wanatia jitihada kwenye ndoto ya kuwa na maisha ya starehe miaka ijayo. Kwa sababu hiyo sote tunajulikana kuwa wachapakazi na washindani katika mitihani yetu. Ni kawaida kwa shule yetu kutupa kazi nyingi sana za kufanya tunapokuwa nyumbani. Kwa hivyo si kawaida kwangu kujipumzisha jioni.

Nina bahati mama yangu ni mwalimu hivyo hunisaidia kazi zangu za shule. Juzi aliniuliza ningependa kusomea nini nitakapofika chuo kikuu. Nilimwambia bado sijaamua kwani nimeanza kujiuliza kama itafaa zaidi kutokuenda chuo kikuu na kukaa nyumbani kwa mwaka mzima. Ingawa ningeweza kufanya kazi, mama yangu anahisi nikifanya hivyo sitarudi tena masomoni kwani nitazoea kujitegemea.

Mazingira

Question 4

Example

M1 Ninaitwa Mwamedu ninafikiri kutunza mazingira ni muhimu.

Question 4a

F1 Ninaitwa Kurwa. Matumizi ya mifuko ya plastiki yalikuwa na athari mbaya kwenye mazingira lakini watu sasa wameelimishwa na kuwa waangalifu.

Question 4b

M2 Ninaitwa Mkude. Kazini kwetu kuna debe la taka kwa ajili ya kuwekea karatasi na kuna jingine la kuwekea maganda ya matunda hivyo ni safi.

Question 4c

F2 Ninaitwa Asha. Miti tuliyoipanda zamani sasa imekuwa mirefu na ina kivuli cha kustareheha.

Question 4d

M1 Ninaitwa Chege. Upungufu wa maji ni tatizo kwa wakulima

Question 4e

M2 Ninaitwa Abushiri. Ndege zinaleta uchafuzi wa hali ya hewa hivyo ninafikiri watu wasiende likizo.

Question 4f

F2 Ninaitwa Doto. Kazi kubwa imefanyika kuhifadhi mazingira na sasa imebaki serikali kuchukua hatua. Jambo litakalowatoa jasho wanasiasa.

Mawasiliano

Question 5

Example

F1 Ninaitwa Emma, nitazungumzia vyombo vya mawasiliano.

Question 5a

F1 Tofauti na zamani ambapo intaneti ilitumika kuwasiliana kutumia kompyuta, simu au mashine nyingine, hivi sasa watu wanatumia vifaa vidogo kama saa ya mkononi.

Question 5b

F1 Ingawa kukutana ana kwa ana ni bora kuliko kutegemea intaneti, angalau intaneti inatuwezesha kutumia video kwenye vifaa tofauti. Ni bora kuliko kusikia sauti kwenye simu pekee.

Question 5c

F1 Mwaka uliopita tulisoma mitandaoni. Lilikuwa jambo la ajabu kuonana kwenye skrini za kompyuta.

Question 5d

F1 Pia tunabandika picha za kupendeza ili kuonyesha shughuli tofauti tunazozifanya. Picha hizo ziliwawezesha rafiki zetu kuona maisha yetu binafsi ingawa faragha imepungua.

Question 5e

F1 Kupata intaneti ambayo si ya polepole wengi huchagua kulipia bili ya mwezi kuhakikisha wana mawasiliano. Zile za kulipia wiki au siku na saa hazina mtandao wa haraka.

Question 5f

F1 Unaweza kutuma ujumbe na kuona kama umesomwa. Unaweza pia kuufuta kama umejuta ulichosema.

Ununuzi

Question 6

- | | |
|----|---|
| F2 | Juma, unajua kwamba maduka makubwa ni tishio kwa maduka madogo? |
| M1 | Ndiyo, nimeona mtaani kwetu maduka madogo yanafungwa na makubwa yanachukua nafasi zao. Hata hivyo, maduka madogo machache pia yana uwezo wa kutoa huduma zao katika majukwaa ya kijamii na kuwa na uhuru wa kuuza wanachotaka kwani hawategemei wanunuzi wanaokuja dukani tu. |
| F2 | Ununuzi unaotegemea intaneti umekua. |
| M2 | Intaneti imetoa nafasi ya kipekee ya kupata wateja wanaotoka duniani kote. Na nimeona wenye maduka haya hutangaza biashara zao kwenye majukwaa tofauti. Faida mojawapo ya nafasi hii ni kuwa hakuna haja ya kutumia pesa nyingi ili kutangaza biashara. |
| F1 | Si rahisi kutuma bidhaa hizo duniani kote. |
| F2 | Wateja walio mbali na duka wanalazimika kulipia kwa bidhaa kuwafikia, jambo linalowakera wengi. Hata hivyo, unaponunua bidhaa za mwuzaji mwenye duka dogo, anaweza kukupa ushauri na kukuuzia vitu vya kipekee. Maduka makubwa huwa na bidhaa nyingi na si rahisi kupata huduma za kitaalamu. |

Maisha mjini na vijijini

Question 7

- M1 Utulivu wa hapa hauna kifani ingawa maoni ya vijana wengi ni kuwa maisha kijijini ni doro. Lela, unapenda kuishi hapa kijijini?
- F1 Sisemi kwamba sipapendi kwani rafiki zangu na mimi tumeishi hapa maisha yetu yote na sisi huzurura karibu na mto ambapo tunaweza kuvua dagaa wadogo tunaowarudisha majini ili waendeleo kuishi maisha yao. Tulipokuwa wadogo, sote tulienda shule ya msingi pamoja kwa hivyo tunajuana vizuri. Hii ilikuwa tofauti tulipoenda shule ya sekondari kwani zote zilikuwa mbali na kijiji. Kijijini si rahisi kuwa na faragha kwani watu hujua yote yanayotokea kwenye maisha ya kila mmoja.
- M1 Kwa kweli maneno yenye kuvutia. Ninakubaliana na wewe Lela. Vipi kuhusu miji, una mawazo gani kuhusu kuishi mjini?
- F1 Labda ningeweza kuishi mjini kama ningekuwa karibu na rafiki na familia yangu. Kuwa mjini kungeniwezesha kufanya mengi ambayo siwezi kufanya hivi sasa. Kwa mfano, mjini ningeweza kuenda kwenye darasa la muziki. Nimevutiwa na muziki maisha yangu yote. Ingebidi nisafiri kwa usafiri wa umma ambapo kuna umati mkubwa. Baba yangu alikuwa mjini hivi karibuni na alijikuta kwenye msongamano wa magari uliochukua dakika tisini badala ya dakika ishirini kutoka hoteli hadi stesheni ya gari moshi. Watu wengi huzungumzia uchafuzi wa hali ya hewa kama tatizo lakini mimi haunisumbui.
- M1 Nimekuelewa.